# SOARING HIGH IN KCPE EXAM

## UTABIRI WA PILI 2021

KISWAHILI LUGHA

**KISWAHILI**
**SEHEMU YA KWANZA: LUGHA**

**Muda:Saa I dakika 40**

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandikia chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki. **Time:1hour** **40 minutes**
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

**NAMBA YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya majibu na usiikunje.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usikunje.
9. Kwakila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D.

   Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

I9. Tumia kiambishi sahihi:•
Darasa __ tajengwa kesho.

A. i B. u C. li D. ki

Jibu sahihi ni C
Katika karatasi ya majibu

Elm [C] [D] I [A m+or Elon«1r El [B] ct Er re tor

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba I9, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwakila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

!!!I

Ecolebooks.com

GEUZA UKURASA

Scanned by CamScanner

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

*ifungu vifatavyo vina nafasi I mpaka I5. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne h*

***ini. Chaguajib lifaalo zaidi kati yayale uliyopewa.***

Hakuna nchi _____1______**kudai i hunu** _____2 itakosa ? wa chakula.

akula ndicho uhai wa watu. Yapo maeneo ambayo _____4_____ na uhitaji mkubwa.

5_____wa chakula hutatizwa na ukosefu wa mvua. Mbegu wanazopanda 6_______**kwa**

**osa unyevu. Wao hutegemea** msimu wa ____T____**kualika. Mbinu kadhaa** za kisayansi

8_______mbegu zinazoweza kupandwa, kuota n a k atika kipindi kifupi mno.

**ote haya ni katika harakati za** I O **na hatari ya kupungukiwa** na chakula.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **1.** A.inaweza | B. zinawezekana | C. inayoweza | D. inaoweza |
| **2. A.** isipokuwa | B. ikiwa | C. ijapokuwa | D. aghalabu |
| **3.** A. uthabiti | B. udhabiti | C. dhabiti | D. thabiti |
| **4.** A. yamekubali | B.zimekumbwa | C. imekubwa | D. yamekumbwa |
| **5. A.** Upaliliaji | B. Uzalishaji | C. Upanzi | D. Ulaji |
| **6. A.** hazichipukizi | B. hazipukutiki | C. hazichipuki | D. zinachipuka |
| 7. A. masika | B. kiangazi | C. kipupwe | D. kaskazi |
| **8.** A. zinavumbua | B. imevumbua | C. zimevumbuliwa | D. zimevumbua |
| 9. A. kukoboa | B. kukomaa | C. kupogoa | D. kudumaa |
| **10.** A. kukabiliwa | B. kukabiliana | C. kukabaliana | D. kukabithi |

Katika mila }______kiafrikani_____hkabisa kumwita mtu kwa

1 3_____mbinja Mwito huo huonyesha dharau. Mwito huo huo ______ 14______ kuwaita wanyama kama vile mbwa. Hii 15______sababu tunapinga tabia ya kutumia mtindo huu wa kuwaita wenzako.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **11.** A. za | B. ya | C. **la** | D.wa |
| 12. A. bora | B. bayana | C. kawaida | D. mwiko |
| **13.** A. kupigia | B. kumpigia | C. kumpiga | D. kupigiana |
| **14.** A. yanatumika | B. ilitumika | C.hutumik:a | D. zinatumika |
| **15.** A. ndivyo | B. ndilo | C. ndio | D. ndiyo |

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

po

Scanned by CamScanner

[redacted]

9

[redacted]

*utoℒa swal fa 16 mpaka 3o cfaguajiu (fi io safifi*

16 Ni sentensi ipi yenye kiambishi ki cha udogo?

A. Ukija utamkuta mwalimu.

B. Tulimwona akilima shamba lake.

C. Kijito hiki kimekauka.

D. Wanafunzi waliimba kitamaduni.

17. Chagua sentensi iliyoandikwa sahihi kisarufi.

A. Pua lake lilikatwa likaunga wajihi.

B. Pua yake ilikatwa ikaunga wajihi.

C. Mapua zake zilikatwa zikaunga wajihi.

D. Mapua yake yalikatwa yakaunga wajihi.

**18.** Kati ya majina yaliyoandikwa ni yapi ni nafaka pekee.

A. Mahindi, Maharagwe, Mtama, Choroko.

B. Mahindi, Matunda, Kiluwa, Mkadi.

C. Adesi, Choroko, Dengu, Peasi.

D. Kunde. Korosho, Pojo, Yungiyungi

19. Neno karib: 'iireiumikaje katika sentensi ifuatayo.

"Mtihani karibu unanukia," Waziri wa Elimu alinukuliwa akisema

A. Nusura

B. Idadi

C. Mahali

D. Wakati

20. Bainisha maneno yaliyopigwa mstari.

Mtoto huyu aliadhibiwa sana, yule mtiifu **alituzwa**

A. Kivumishi, kirejeshi, kihisishi, kiwakilishi

B. Kirejeshi, kivumishi, kiashiria, kitenzi

C. Kiashiria, kielezi, kiwakilishi, kitenzi

D. Kiashiria, kivumishi, kimilishi, kitenzi

**21. Kanusha** sentensi ifuatayo:

Mwalimu ajaye amefika

A. Mwalimu ajaye asifike

B. Mwalimu ajaye hakufika

C. mwalimu asiyekuja amefika

D. mwalimu ajaye hajafika

**22. Musa aliguria** Sokomjinga. Kisawe cha neno lililopigwa mstari ni?

A. alihamia

B. aliuzia

C. alikodeshea

D. alijengea

23. Kati ya sauti zifuatazo ni ip i nayojumuisha orodha ya sauti ghuna

A. f, l, sa

B. m, s, th

C. dh, ng. b

D. ha, f, sa

**24.** Chagua usemi wa taarifa wa:

"Njooni shuleni kesho na wazazi wenu," Mwalimu alituambia.

A. Mwalimu aliwaambia waende shuleni na wazazi wao siku iliyofuata

B. Mwalimu alituamuru tuende shuleni siku ifautayo na wazazi wetu

C. Mwalimu alituambia njooni shuleni kesho na wazazi wenu.

D. Mwalirnu alituarnuru tuende shuleni siku iliyofuata na wazazi wetu

**25.** Tegua kitendawili kifuatacho: Manne Manne hadi Pemba

A. Gari

B. Magurudumu

C. Usingizi

D. Mkokoteni

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Scanned by CamScanner

26. Elezea tarakimu ifuatayo husomwaje?
13,003
A. Elfu kumi na kwni na tatu
B. Elfu kumi na tatu
C. Elfu kumi na kumi na tatu
D. Kumi na tatu elfu na tatu

27. Chagua sentensi iliyo katika nafsi ya pili kwa wingi?
A. Mimi napenda kulima wao hawapendi.
B. Sisi sote twatakikana uk:umbini.
C. Kimani ni mtoto mzuri ilhali wewe nimtundu.
D. Nyinyi nyote mtashiriki katika mchezo wa kuigiza.

28. Maria alifunga nikaha na Juma. Je Maria atamwitaje ma.make Juma?
A. Mavyaa
B. Bavyaa
C. Mamamkwe
D. Mk.azahau

**29.** Ni salamu zipi ambazo hutolewa wakati wa maombolezi
A. Asalam aleikum
B. Chewa
C. Makiwa
D. Kongole

30. Ni orodha ipi ya maneno inayoonyesha nomino wingi.
A. Makabati, majedwali, maclawati, mavaz1
B. Maji, mafuta, manukato, marashi
C. Matofaa, motokaa, matufaha, mafiga
D. Matatu, matwana, makao, magurudumu

Ecolebooks.com

STANDARD

8

Scanned by CamScanner

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

*Soma kifungu kifatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.*

Teknolojia mpya ni tawi la maarifa linalohusiana na sayansi kwa upande mmoja na uhandisi (Uinjinia) kwa upande mwingine. Saynsi ni elimu inayotokana na uchunguzi na majaribio katika maabara. Nao uhandisi ni ujuzi wa kuunda mitambo. Maarifa ya sayansi yanapotumiwa kutengeneza vitu viwandani, hali hii inakuwa teknolojia

Zao mojawapo la teknolojia mpya ni simu tamba. Watu sasa wanawasiliana na jamaa zao walio mbali. Akina nyanya wanapopanda njugu, kupalilia migomba, kukama ngamia na kukuna nazi, wanaweza kuzungumza na wajukuu wao walio Uingereza Uchina na kwingine kule. Hakuna mahali ambapo hapajafikiwa na teknolojia mpya. Tukitembelea baadhi ya nyumba tutaona vifaa kama vile tanuri la miale. Vilevile kuna jiko la mvuke ambalo linapika maharagwe yakaiva kwa dakika chache tu. Majokofu nayo yanatuwezesha kuhifadhi vyakula bila kuharibika. Hata maiti na mizoga inaweza kuhifadhiwa kwa miaka mingi kwa ajili ya utafiti bila kuoza katika ufuo wa mochari

Kwa upande wa kilimo, teknolojia imefanya makubwa. La kustaajabisha ni mtu mmoja kulima eneo kubwa la shamba kwa trekta. Halafu akapanda kwa tandazi, akanyunyizia dawa kunyausha magugu, akavuna na kukoboa mahindi akiwa peke yake. Siku hizi inawezekana kukuza mimea na kufuga wanyama wanaokomaa kwa muda mfupi na kutoa mazao maradufu

Kwa sababu ya knolojia mpya. Teknoljia imewezesha watu kuvumbua aina nyingi za nishati . Badala ya kutegemea umeme unaotokana na maji tu, sasa watu wanatumia mvuke, nguvu za upepo na nishati ya jua kupata umeme. Kwa sababu hii hata mababu zetu vijijini wanatazama televisheni bila shida au wahaka.

Kwa upande mwingine, teknolojia ina madhara yake. Kwa mfano, uundaji wa silaha kali unaendelea kuwaangamiza watu wengi. Mabomu ya kitonoradi yaliyoangushwa Hiroshima na Nagasaki Japani mwaka wa 1945 ni zao la kisayansi. Haya yaliwaua watu wengi na madhara yake bado yanadhihirika hata katika maumbile ya watoto wanaozaliwa na upungufu. Tena magaidi na wahalifu wa kimataifa wanatumia teknolojia mpya kuimarisha mbinu zao *za* kutenda maovu. Isitoshe, inawezekana kutumia teknolojia kuagiza benki kutuma pesa nje ya nchi bila mwenye hazina kujua.

Wahalifu wanawezakusikiliza mawasiliano ya watu kwa simu hata ikiwa ni baina ya polisi. Kisha matatizo mengi ya kiafya yasemekana yanatokana na vyakula ilivyokuzwa kwa kutumia teknolojia mpya. Katika usafiri kuna gari moshi lenye kutumia stima badala ya makaa. Hili ni zao la teknolojia mpya. Ingawa mwendo wake ni wa kasi kasi hiyo ya stima huweza kusababisha ajali mbaya mno.

31. Teknolojia mpya ni tawi linalohusiana na
    A. Uchunguzi wa maabarani
    B. Sayansi na uhandisi
    C. Ujuzi wa kuunda mitambo
    D. Utengenez.aji wa vitu viwandani

32. Baadhi ya mazao ya teknoloji ni
    A, Chungu, seredani,na stovu
    B. Stuli, meza, kiti na kabati
    C. Rununu, trekta, mikrowvu na tandazi
    D. Patasi, tupa, bisibisi na sepetu

Ecolebooks.com



Scanned by CamScanner

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

33. Ni sentensi ipi si sahihi kulingana na kifungu?
A. Maarifa ya sayansi hayatumiwi kutengeneza vitu viwandani
B. Teknolojia imewezesha watu kuvumbua aina nyingi za nishati
C. Garimoshi hutumia stima badala ya makaa
D. Wanavijiji wanawasiliana na jamaa zao walio mbali

34. Neno kuhifadhi limepigwa mstari maaoa yake ni____
A. kulaza
B. kufichua
C. kuharibu
D. kulinda

35. Taja baadhi ya vifaa vya mekoni ambavyo ni vya teknolojia
A. Tanuri, stovu najokofu
B Mikrowevu, seredani, stovu
C. Jokofu, tanuri najiko la mafiga
D. Jokofu, tanuri najiko la mvuke

**36.** Kisawe cha neno nishati ni __ __
A. Kawi
B. Mwangaza
C. Mvuke
D. Joto

37. Maumbile ya watoto **wanaozaliwa yana** upungufu kwa sababu ya____
A. Risasi
**B.Mabomu**
C. Mizinga
D. Manowari

**38.** Kulingana na makala haya sentensi ipi nisahihi
A. Mtu hawezi kutuma pesa nje ya nchi.
B. Mabomu ya kitonoradi yaliyorushwa hayakuleta madhara.
C. Mtu anaweza kuagiza benki kutuma pesa nje ya nchi.
D. Magaidi hawawezi kutumia teknolojia mpya kuimarisha mbinu zao.

39. Kwa mujibu wa aya ya mwisho madhara yafuatayo yamezungumziwa ila ya
A. Afya
B. Mawasiliano
C. Usafiri
D. Elimu

**40.** Kichwa mwafaka cha kifungu hiki ni
A. Teknolojia
B.Elimu
C. Afya
D. Madhara

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 4I mpaka 50.*

Shani alikuwa ametoka kazini akiwa mchovu wa mwili na moyo. Baada ya kujimwagia maji, alijipweteka kitini na kufungulia runinga yake kutazama yapitayo nchini. Mara tu baada ya kufungua kidude hiki, alisalimiwa na sauti nyororo ya kike ikitangaza, "Rais amemteua Bi. Maua kuwa katibu mkuu wa wizara ya fedha. Uteuzi huu unatekelezwa maramoja."

Shani alisikiza tangazo hili kwa mshangao wa ajabu. Alitaka kumwuliza mtangazaji huyu kama kweli aliyokuwa ametamka yalikuwa ya kweli lakini alitanabahi kuwa hicho kilikuwa kisanduku tu cha kutolea habari. Maswali mengi yalimpitia akilini. Huyu si yule Maua maskini tuliyesoma naye kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne? Imetokeaje ameweza kupata wadhifa wa aina hii? Kwani baada ya kidato cha nne aliweza kupata karo ya kumwezesha kwenda chuo kikuu? Itakuwaje mimi niliyekulia nasaba bora niwe ndimi wa kuishi maisha ya uhitaji naye kutononoka hivyo.

Ecolebooks.com



Scanned by CamScanner

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Wakati Shani alipokuwa akijisaili hivi, alikuwa ameghafilika kuwa yeye na Maua walikuwa watu tofauti. Shani akiwa shuleni alikuwa hazingatii masomo yake. Maua alipokuwa akidurusu, **Shani** alikuwa akipitisha muda wake akiota ndoto za kila aina. AJishindwa kabisa kumamia cha **mvunguni kwani wazazi wake walimpa kila alichotaka .Kila** mara alipofungua shule, sanduku

lake lilipakia shehena hadi likalalamika. Shani alizoea kulivuta sanduku lake kulitembeza kote bwenini huku akiwafanya wenzake kuajabia na kuumezea mate utajiri huu. Mara nyingine aliweza kumfaa Maua kwa vifaa vya hapa na pale kama vile sabuni, shashi na hata vyakula. Maua kila mara alishukuru moyoni ila alimhuzunikia huyu mwenzake ambaye daima alikuwa akitaradhia waza.zi wake.

Kila mara Maua alikuwa akimshawishi Shani amakinike katika masomo yake lakini Shani alidai kuwa yeye hakuwa na kipawa hicho. Alisema kuwa kwa sababu ya urcmbo wake aliazimia kuwa mhudumu katika ndege pindi amalizapo kusagika na elimu ya kidato cha nne. Wasichana hawa wawili walifanya mtihani wao. Kama ilivyotarajiwa Maua alitia fora akawa mwanafunzi wa kwanza shuleni mwao. Hali yake ya baadaye ikawa inaweza kutabiriwa. Shani naye alichumia kivulini akaliajuani. Maazimio yake ya kuwa mhudumu katika ndege yalianza kuyeyuk akaona haya kuwataka wazazi wake kumtafutia nafasi katika shirika la ndege.

Matumaini yake yalipotumbukia nyongo, Sham alijiunga na chuo kimoja nchini ambapo alijifunza uhazili. Akaona kwamba ilimbidi kujitegemea kwani wazazi wake sasa walik a na mzigo mkubwa wa kuwalea wana wao. Alifanya 'idii katika mafunzo haya. Alifuzu mwaga mhazili na **kuanza** kazi katika shirika moja la simu. Kwa vile nchi ilikuwa katika harakati z k iikuza kiteknolojia, ilimwisia vigumu Shani kuomba mshahara mkubwa kwa hofu kwamba unga wake kwani tangu hapo wakubwa wengi hawakuhitaji wahazili. Ikabidi kujikucho atapo. Zile ndoto alizokuwa nazo za kuishi katika nyumba kubwa kama ya wazazi wake ziliyeyuka kama barafu wakati wajoto kali. Alijipata anaishi na wenzake katika chumba kimoja amb:cl ndicho kilichogawanywa kuwa cha malazi na sebule.

Maua kwa upande wake, baada ya kufanya vyema katika mtihani wa kidato ch nte aliona jahazi lake likitia nanga kwenye ufuo usio na matumaini. Elimu ya chuo kikuu wakat huo ilikuwa ikigharimu fedha na alijua fika kuwa wazazi wake wasingeweza kumwauni kwa lolote. Alikesha usiku akigalagala kitandani asiambulie lepe lolote la usingizi. Hatimaye alipata suluhisho.

Aliamua kuandamana na babake katika afisi moja ya umma ambapo ufadhili wa masomo ya juu ulitolewa. Maua kwa weledi wake wa lugha aliweza kuwashawishi wakuu wa idara l umpa udharnini wa masomo ya chuo kikuu.

Baada ya kuamkia bahati hii, Maua hakutazama nyuma. Aliabiri chombo, akapaa juu angani na kujipata Marekani akisomea uhandisi wa mitambo ya komputa. Baada ya kuhitimu, Maua hakubaki Marekani licha ya kuwa mashirika mengi yalikuwa yamemwahidi nafasi za kazi. Alirejea nyumbani kuendeleza shughuli za ujenzi wa taifa. Maua alilakiwa na kupewa nafasi ya kazi katika wizara ya fedha. Kwa sababu ya mapenzi yake kwa familia na nchi yake alifanya kazi kwajitihada kubwa. Wakuu wake waliweza kuona bidii zake za mchwa, akapanda kidato kimoja cha ngazi baada ya kingine. Ingawa kila mara alikumbuka rafiki yake Shani ambaye licha ya kiburi chake wakiwa shuleni aliweza kumfaa kwa mengi, hakuweza kuwasiliana nayc kwani hakuwa na anwani yake.

Ecolebooks.com



Scanned by CamScanner

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Wakati huu Shani alipokuwa akiungulika kwa macbungu juu ya ufanisi wa Maua, Maua alikuwa kajawa na bashasha isiyo na kifani kwa kupata cheo hiki ambacho kwa kweli alikuwa anastahi li kukipata. Moyoni aliwaza kuwa lazima amtafute rafiki na mhisani wake wa zamani.

**41.** Kulingana na kifungu:

A. Shani alikuwa ameteuliwa na Rais kuwa katibu mkuu wa wizara ya fedha.

B. Bi Maua alikuwa mtangazaji mwenye sauti. nyororo.

C. Shani alikuwa amelelewa kwa familia yenye uchochole mwingi.

D. Wadhifa aliotunukiwa Bi Maua ulikuwa wa kutononoka.

**42.** Katika aya ya tatu wazo sahihi kulingana na mwandishi ni:

A. Shani alitia bidii masomoni.

B. Shani na Bi. Maua waliota ndoto za kupitisha muda.

C. Bi Maua na Shani walikuwa wanasoma shule ya bweni ya wasichana.

D. Shani na Maua walikuwa watu tofauti kitabia

**43.** Kulingana na kifungu maazimio ya Shani yalikuwa?

**A. Kutia** fora na kuwa rubani.

B. Kuhudumu katika ndege kwa vile alikuwa mrembo.

C. Masomoni kwa kuwa alichumia juant.

D. Alikuwa na kipawa masomoni.

**44.** Shani alihofia kuomba mshahara mkubwa katika shirika alilofanya kazi kwa sababu?

A. Alijikuza kiteknolojia

B. Wakubwa wengi hawakuhitaji wahazili.

C. Ndoto yake ilikuwa imetimia.

D. Hakutaka makuu.

**45.** Msemo kujikuna ajipatapo umetumika **kuwa** na maana ya:

C Kuwa mkaidi

A. Kadri ya uwezo wako

B. Kuvumilia shida zako

D. Kukosa hali.

**46.** Jahazi lake likitia nanga kwenye ufuo usio na matumaini ni sawa na:

A. Tia taabani

B. Tia katika jambo geni

C. Fika mwisho

D. Fika miaka ya uzeeni

**47.** Kulingana na kifungu ukakamavu wa Bi. Maua unajitokeza wazi wakati?

A. Alipojipata Marekani akisomea uhandisi.

B. Alipokuwa akiwaza kumtafuta Shani amsaidie.

C. Alipowashawishi wakuu wa idara kumpa udhamini wa masomo, D. Alipoandamana na babake.

**48.** Ni mfuatano upi wa matukio ufaao kwa mujibu wa kifungu kuhusu Bi. Maua?

A. Shute ya upili, chuo kikuu, ng'ambo, kurejea nyumbani, waziri wa fedha.

B. Chuo kikuu, ng'ambo, waziri wa fedha.

C. Shule ya upili, chuo cha uhazili, shirika la simu, ng'ambo.

D. Shule ya upili, ng'ambo, chuo kikuu, shirika la simu.

**49.** Ni methali ipi inayohusiana na hulka ya Bi. Maua?

A. Aliye juu mngojee chini.

B. Ukiona vyaelea vimeundwa.

C. Cha kuvuja hakina rubani.

D. Mtegemea cha nduguye hufa

**50.** Kichwa mwafaka kinachofaa kuelezea taarifa hii ni?

A. Bidii ya Bi. Maua

B. Bidii ya Shani

C. Ziara ya Maua

D. Urafiki wa kejeli.



Scanned by CamScanner